

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



TANGAZO

ZABUNI MBALIMBALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

KWA AJILI YA

**HUDUMA YA ULINZI NA UKUSANYAJI WA USHURU WA
CHOO CHA STENDI, SABASABA NA SOKO KUU**

KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

MWALIKO WA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi inatangaza zabuni za huduma ya ulinzi kwenye majengo ya Manispaa na ukusanyaji wa ushuru choo cha stendi, sabasaba na soko kuu kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Juni, 2020 kama ilivyoainishwa hapo chini:-

ZABUNI NA. LGA/053/2019/2020/HQ/NS/08: HUDUMA YA ULINZI

Idara	Idadi ya Walinzi	Kiasi kwa Mlinzi kwa mwezi	Jumla
Afya (Ofisi ya Afya 1, Zahanati ya nachingwea 1, Zahanati ya Manispaa 1 na Kliniki ya Manispaa 1)	4		
Uwanja wa Ilulu	1		
Ujenzi	3		

Utawala (Soko kuu 3, Ofisi kuu 1 na Soko la Sabasaba 1)	5		
Mipangomiji (DDC)	1		
Mifugo (Machinjio)	2		
Shule ya Msingi Mpilipili	2		
Maktaba ya Mkoa	1		
Ofisi ya Ugavi, Maendeleo ya Jamii na Mifugo	1		
Nyumbani kwa Mkurugenzi	1		
JUMLA	21		

ZABUNI NA. LGA/053/2019/2020/HQ/NS/10: UKUSANYAJI WA USHURU WA CHOO CHA STENDI, SABASABA NA SOKO KUU

MASHARTI YA MAOMBI YA ZABUNI:

- Mwombaji lazima awe na ofisi inayotambulika, anuani ya posta na namba ya simu.
- Mwombaji awe na Leseni hai ya Biashara na pia leseni ya zabuni inayotolewa na Mamlaka husika, TIN namba pamoja na nyaraka nyingine muhimu zinapaswa pia kuwasilishwa.
- Mwombaji anatakiwa kuambatanisha taarifa ya Benki (Bank statement) ya mwaka mmoja hadi 30/04/2019 ili kuthibitisha uwezo wake kifedha.
- Ada ya Tshs.50,000/= kwa zabuni / ilipwe katika akaunti ya Makusanyo ya ndani ya Manispaa. Mzabuni atapaswa kuambatanisha stakabadhi ya malipo wakati wa kuwasilisha zabuni yake.
- Halmashauri ya manispaa ya Lindi haitalazimika kukubali zabuni ya chini kabisa au ya juu.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI HAYO:

Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa kwenye bahasha na kuwekwa lakiri (seal). Juu ya bahasha iandikwe Mfano: Zabuni na. LGA/053/2019/2020/HQ/NS/08 (Huduma ya Ulinzi), na itumwe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu, Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi
S. L. P 1070

LINDI

Zabuni zinaweza kupelekwa kwa mkono au posta na siku ya mwisho kupokea zabuni hizo ni siku ya Ijumaa tarehe 21/06/2019 saa 4.00 asubuhi na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi muda mfupi baada ya zabuni kupokelewa mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria.

Wote mnakaribishwa.


Satura J.M

MKURUGENZI WA MANISPAA YA LINDI

**MKURUGENZI WA MANISPAA
LINDI**